SHULE YA SEKONDARI PHILIP MANGULA

S.L.P 699 NJOMBE

BARUA PEPE ………………..

Mob 0767809402

Tarehe ………………..

Kumbu Na PMSS/JI/06/01/11

Jina la Mwanafunzi …………………………………………..

………………………………………………………………………….

S.L.P ………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………..

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PHILIP MANGULA WILAYA YA WANGING'OMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 shule ya sekondari Philip Mangula ipo umbali wa km 25 magharibi /mji NJOMBE.

Usafiri wa basi kutoka mjini NJOMBE unapatikana katika kituo cha mabasi cha NJOMBE. Nauli ni Tsh. 3000.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare za shule**

a) Sare ya shule kwa wavulana na wasichana maelezo ya mshono vimeambatanishwa pamoja na kitambaa

**3.0 Sheria na kanuni Muhimu za shule hii**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais- Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma.

**3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
e) Kupiga au kupigana
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi, vifaa vya umeme kama Heater, radio n.k

**4.0 Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

a) Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukabiliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewana shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**………………………………………………..**

**MKUU WA SHULE**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be complete by a medical officer in respect of all form 1/form V entrants and new school employees

Full Name: …………………………………………………………………………………………

Age ……………………….. Years. Sex: ……………………………………………………………..

Blood Count (Red and white): ……………………………………………………………………

Stool Examination: ………………………………………………………………………………

Urinalysis: ……………………………………………………………………………………….

Syphilis Test: ……………………………………………………………………………………

T.B. Test: ……………………………………………………………………………………….

Eyes Test: ………………………………………………………………………………………

Ears : …………………………………………………………………………………………...

Chest : …………………………………………………………………………………………

Abdomen: ………………………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION**:- eg Physical defect of impairment (s),

Infections, Chronic or family disease

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit/unfit to pursue his/her lessons/ duties as required.

Signature
…………………………………………………………………………

Designation………………………………………………………………………..

Date ………………………………………. Station
………………………………………………………………………..

Note: Medical officer: At the time of examination, please treat the individual for any ailments you note.

Pupils/ Employee: This complete form should be sent to the school with your acceptance form, or brought when you come to the school. No pupils any Errol, nor person any employed with certification or physical fitness.

- ❖ Delete as necessary

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI.**
**PHILIP MANGULA SEKONDARI.**
**FOMU YA KUKUBALI NAFASI.**

**A. MWANAFUNZI.**

**JINA LA MWANAFUNZI: ______________________________________________**

**ANWANI: _________________________________________________________**

**TAREHE: _________________________________________________________**

Mimi ____________________________________________ nimekubali kujiunga na shule ya sekondari Philip Mangula baada ya kusoma na kuelewa sheria, maelezo na maagizo ya shule. Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria na taratibu za shule kama nitakavyoelekezwa.

**Saini ya mwanafunzi : _______________________________**

**Tarehe : __________________________________________**

**B. MZAZI/MLEZI**

Mimi _________________________________ nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa yanayohusu mtoto wangu. Nimekubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo, Naahidi pia kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia.

**Saini ya Mzazi: ___________________________________________**

**Tarehe: ________________________________________________**

**WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI**

**MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI**

**A: 1.** Jina la mwanafunzi : …………………………………………………………………

**2.** Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………….

**3.** Mahali alipozaliwa (Wilaya): ……………………………….. Mkoa: ……………

**4.** Dini: …………………………………… Dhehebu ………………………………

**B: 1. J**ina la mzazi anayekutunza: ………………………………………………………

2. Kazi ya mzazi/Mlezi:…………………………………………………………….

3. Anuani ya mzazi/Mlezi: . ……………………………………………………….

4. Mahali ambapo anaishi Mzazi/Mlezi ……………………………………………

Kijiji /Mji ……………………………………………..Kata: ………………………

Mkoa :…………………………………………………………………………

C. Majina ya ndugu wengine wanaohusika na malezi ya mwanafunzi huyo:

1. Ndugu …………………………………………………………………...
   Anuani : ………………………………………………………………
2. Ndugu : ………………………………………………………………
   Anuani :………………………………………………………………

D: Anuani za ofisi ya Mtendaji Kata na Mwenyekiti Kijiji /mtaa ambako mzazi au mlezi wa mwanafunzi anaishi.

1. Afisa Mtendaji Kata:
   ……………………………………………………………………………

   Kata ya: ……………………………………………………………………………

   Anuani : ……………………………………………………………………………..

2. Mwenyekiti wa
   Kijiji/Mtaa………………………………………………………………………………
   ……….
   Kijiji cha /Mtaa ………………………………………………………………
   Anuani : ……………………………………………………………………………

Zingatia: Tafadhali ijaze fomu hii kwa uangalifu.

Futa isiyohusika

**2:5 SARE**

**WAVULANA**

- Suruali mbili (02) za rangi ya Dark Blue namba moja  zenye turn up (zisizo model) kwaajili ya darasani.
- Masharti mawili (02) mikono mirefu
- Suruali mbili (02) za rangi ya ugolo namba moja kwaajili ya kazi za nje
- T-shirt mbili (02) za kutanguliza ndani au Vest/sing land nyeupe
- T –shirt mbili (02) za blue zenye shingo ya duara zisizo na maandishi (kwaajili ya kazi za nje
- Viatu vyeusi vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu pair mbili (02)
- Ndoo mpya ndogo rangi nyeusi kwaajili ya kuogea (tafadhali rangi ya ndoo izingatiwe kwa kuwa kila kidato wana rangi yao)
- Kombe kubwa (mug)  lenye mshikio la lita moja kwaajili ya kuogea (isiwe lita ) pamoja  na dodoki la kujisugulia
- Sahani moja, kijiko kimoja na kikombe kimoja cha nusu lita kwa ajili ya uji(sio kontena
- Mashuka mawili (02) yenye rangi ya light blue ( tafadhali rangi izingatiwe)
- Soksi pair mbili (02) za khaki au nyeusi
- Nguo za ndani za kutosha angalau sita au zaidi
- Bukta za kuvaa ndani angalau tatu au zaidi
- Taulo kubwa kwa ajili ya kuogea
- Mkanda wa ngozi mweusi kwa ajili ya kuvalia suruali
- Sabuni za kufulia kuanzia miche mitatu au zaidi
- Mafuta ya mgando ya kupakaa kopo kubwa moja (sio lotion)
- Miswaki miwili na dawa ya meno kubwa
- Leso mbili (02)
- Kitana kwa ajili ya kuchania nywele
- Kandambili kwa ajili ya kuogea
- Raba kwa ajili ya michezo
- Track suit dark blue mistari myeupe kwa ajili ya michezo
- Godoro la futi mbili na nusu aina ya Dodoma au Tanfoam
- Gillete mashine kwa ajili ya kunyolea / usafi binafsi
- Sweta rangi ya Agua Green V uzi umeambatanishwa kwenye fomu hii.
- Aje na jembe likiwa kwenye mpini
- Aje na Tranka
- Aje na bunda  la karaasi (Ream)
- Aje na kamusi ya kiingereza (English dictionary)

**2.5 SARE**

**WASICHANA**

- Suruali mbili (02) za rangi ya Dark blue zenye Turn up(zisizo model zenye upana wa wastani)
- Brouse mbili (02) zenye mikono mifupi zenye malinda kuanzia kiunoni yanayochanua kufika usawa wa magoti na kola pana za kuanguka kitambaa koshibo usipoelewa mafundi wanapatikana karibu na shule.
- Magauni mawili (02) marefu yenye mshono wa soro ya rangi ya zambarau na orange kitambaa cha magauni ni koshibo
- T –shirt mbili (02) nyeupe za kutanguliza ndani darasani
- Viatu vyeusi (02) vyenye kamba (gidamu) visivyo na kisigino kirefu.
- Ndoo mpya ndogo rangi nyeusi kwaajili ya kuogea (tafadhali rangi ya ndoo izingatiwe kwa kuwa kila kidato wana rangi yao)

- Kombe kubwa (mug) lenye mshikio la lita moja kwaajili ya kuogea (isiwe lita ) pamoja na dodoki la kujisugulia
- Sahani moja, kijiko kimoja na kikombe kimoja cha nusu lita kwa ajili ya uji(sio kontena
- Mashuka mawili (02) yenye rangi ya light blue ( tafadhali rangi izingatiwe)
- Soksi pair mbili (02) nyeupe
- Nguo za ndani za kutosha angalau sita au zaidi
- Skin tight za kuvaa ndani kuanzia tatu au zaidi
- Brazia (sindiria) au top za rangi nyeupe na nyeusi
- Sabuni za kufulia kuanzia miche mitatu au zaidi
- Mafuta ya mgando ya kupakaa kopo kubwa moja (sio lotion)
- Miswaki miwili na dawa ya meno kubwa
- Leso mbili (02)
- Kitana kwa ajili ya kuchania nywele
- Kandambili kwa ajili ya kuogea
- Raba kwa ajili ya michezo
- Track suit dark blue mistari myeupe kwa ajili ya michezo
- Godoro la futi mbili na nusu aina ya Dodoma au Tanfoam
- Underskirt (02) kwaajili ya kuvaliamagauni
- Kanga mbili au vitenge kwa ajili ya kuogea
- Gillete mashine kwa ajili ya kunyolea / usafi binafsi
- Pedi kuanzia pakiti nne (04) au zaidi
- Sweta rangi ya Agua Green V uzi umeambatanishwa kwenye fomu hii.
- Aje na jembe likiwa kwenye mpini
- Aje na Tranka
- Aje na bunda la karaasi (Ream)
- Aje na kamusi ya kiingereza (English dictionary)

**2.3 CHAKULA**

- Mahindi debe kumi (10) za lita 20 yaliyokauka vizuri na yasiyobunguliwa na wadudu
- Mchele kilo ishirini (20kg) usiwe usiovunjika (sio chenga)
- Maharage kilo hamsini (50kg) yasiyo mchanganyiko (tafadhali zingatia hili)
- Fedha taslimu shilingi laki moja na thelathini (130,000) kwa ajili ya viungo, sukari, nyama, mafuta, mboga za majani, chumvi, vifaa vya kupikia na posho za wapishi wanne (04) ikumbukwe kuwa shule yetu haina chakula maalum (special diet) kwa wanafunzi ikiwa mwanao ana mahitaji maalum ya chakula hatapata huduma hiyo hapa.

**NB: Malipo yote ya fedha yalipwe benki kwa akaunti zifuatazo:**

1. **Michango ya Hosteli NMB tawi la njombe akaunti namba 60601000024 PHILIP MANGULA SEKONDARI tafadhali taja jina la mwanafunzi anayelipiwa (130,000/=)**
2. **Wanafunzi wanaotoka nje ya kata ya Imalinyi, wazazi/walezi wao wanachangia ujenzi wa miundo mbinu (ukumbi, bweni, n.k) fedha Tshs 40,000/= au nguvu kazi au vifaa vya ujenzi kila mwaka. NMB tawi la njombe akaunti namba 60606600337 KAMATI YA UJENZI PHILIP MANGULA SEKONDARI. Leta risiti ya kuwekea fedha benki (BPS) Kwa uthibitisho.**
3. Fedha taslimu haipokelewi tafadhali zingatia maelekezo.